

U F U N U O (Sehemu ya 3)

Wagalatia 1:11-20... Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu wala sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa Ufunuo wa Yesu Kristo. (Mstari 12).

Hebu tusikilize zaidi kile Nabii wa Mungu alichosema juu ya ... Ufunuo” mwanaume au mtu anapokuwa amekutana hasa na Mungu, akiwa na Imani halisi iliyofunuliwa kwamba Mungu yupo (waebrania 11:6), hakuna kitu chochote, hakuna muda, hakuna popote, pawezapo kumtenga mtu huyo na Mungu wake. Ninaamini ni Paulo alisema, hakuna mashindano, wala njaa, wala dhiki, wala kiumbe chochote, au kifo au chochote kiwezacho kututenga sisi na upendo wa Mungu ulio ndani ya Kristo Yesu” (Warumi 8:35-39).

Umetia nanga na uko salama ndani yake kwa sababu ulikusudiwa uzima. Lakini Shetani ingawa anaweza kumyumbisha kidogo, na kumkaba yeye, na kumfanya alifanye hilo. Lakini unaona, Ayubu akiwa na ufunuo wake mkamilifu wa Mungu na vile Mungu alivyokuwa, na vile Mungu alivyompenda yeye, alisubiri. Haijalishi mazingira yalikuwa ya namna gani, alisubiri imani yake iweze kuthibitishwa, kwa sababu alikuwa amemshikilia Mungu, Ufunuo (Ayubu 19:25-27).

Sasa, ninyi watu wagonjwa, watu mliopooza, au ninyi mlilo na uhitaji wa Mungu, mnapoweza kupata aina hiyo ya ufunuo kwamba umehesabiwa haki (Warumi 8:30, 1Kor. 6:11), Unapohesabiwa haki kuomba kitu kile unachoomba, na kwamba anawapa thawabu wale wanaomtafuta yeye, hakuna chochote kiwezacho kukutenganisha na Imani hiyo ambayo imetia nanga ndani yako. Unaona? Lakini kwanza haina budi kuwa imefunuliwa kwako. [1]

Mungu anaposema kuwa ni hivyo, basi hivyo ndivyo ilivyo hivyo ndivyo. Kama Mungu ameweka ahadi, shikilia hilo kwa nafsi yako. Kama unaweza kuliamini hilo, shikilia..... kama huamini kaa mbali na hilo litakuumiza. Lakini kama unaliamini shikilia hilo litakuleta kwenye ushindi (1Yohana 5:4), kwa hakika hasa kama ilivyo Dunia. [2]

Sasa Imani ni ufunuo kutoka kwa Mungu. Ni ufunuo. Kwamba amelifunua kwako kwa Neema. Siyo chochote ulichofanya. Wewe hukufanya kazi yoyote mpaka kupata imani. Kamwe huna imani. Umepewa hiyo kwa neema ya Mungu. (1Petro 1:13)... na mungu analifunua kwako, kwa hiyo imani ni ufunuo. Na Kanisa lote la Mungu linajengwa kwenye ufunuo.

Na Imani inakuja kwa kusikia, Ufunuo unakuja kwa kusikia ni ufunuo wa mtu binafsi, ambao ni Imani, Imani ambayo imefunuliwa.

Mhuduma mmoja wa Kibaptist aliniambia, muda sio mrefu uliopita alisema...., Mimi siwezi kukubali ufunuo” Nikamwambia, Basi huwezi kuikubali Biblia. Huwezi ukamkubali Kristo, kwa sababu yeye ni ufunuo wa Mungu. Yeye ni ufunuo wa Mungu katika mwili” (1Tim.3:16), kwa hiyo, Kanisa lote limejengwa juu ya ufunuo (Matayo 16:13-20).

Habili kwa imani, ufunuo (hakuna Biblia iliyokuwa imeandikwa siku hizo)... Habili, kwa Imani alimtolea Mungu sadaka iliyo bora kuliko ile ya Kaini. Ambayo Mungu alishuhudia “Alikuwa ni mwenye haki” kwa namna gani? Kwa imani, namna gani? Kwa ufunuo! Kwa ufunuo, Habili alimtolea Mungu sadaka iliyobora, kwa sababu ilifunuliwa kwake kwamba haikuwa matunda ya shambani, ilikuwa ni damu (Mwanzo 4:3-4).

Hiyo ndiyo maana watu wengine wanaweza kuliamini hilo na wengine hawawezi kuamini hilo, wengine wanajaribu kujifanya kuamini hilo.

Katika kusanyiko la watu, mahali ambapo upo mstari wa maombi, utaona ya kuwa wengine..... na wote ni watu wazuri, watasema kuna wanaojaribu kwa nguvu kuliamini hilo, wakijaribu kutenda kitu fulani wapate hilo. Wengine hawawezi kufanya hivyo kabisa. Na wengine, ni kwa neema tu, wanapewa tu hilo (1Petro 1:13). Sasa, hapo kuna tofauti unaona? Hilo linafanya hivyo, Huo ndio ufunuo halisi kwa sababu imani ni Ufunuo kutoka kwa Mungu. Ni lazima ifunuliwe kwanza.

Yesu alilieleleza hili kwa wazi aliposema, hakuna mtu awezaye kuja kwangu asipovutwa kwanza na Baba yangu, au Nifunuliwe kwake kwanza (Yohana 6:43-44). Nataka kukuambia kitu kingine tena, tenda katika mdundo huo, muda ule kidogo wa akiba, kama Joshua alivyofanya, kama Mariamu Magdalene, wote hawa. Wakati ule tu jambo fulani linapofunuliwa kwako, likamate, lishikilie hilo, muda ule mdogo wa akiba.

Sasa, siwezi kukufanya wewe uamini, wala huwezi kujifanya mwenyewe uamini. Mungu ndiye awezaye kukupa wewe hilo.

Kuamini ni kipawa cha Mungu (Waefeso 2:8). Siyo imani yako. Imani ya Mungu (Marko 11:22), Imani yako ya kiakili inaweza ikaliamini hilo, vizuri, lakini ni mpaka imani ya Mungu iwe ndani ya Moyo.... (Wagalatia 2:19-21, Unaona, Imani yako ya kiakili inaweza ikalikubali hilo, fanya hivyo na uendelea kuamini kwa moyo wako wote mpaka Mungu alifunue hilo kwako. Unaona? Endelea tu kuamini mpaka Mungu amelifunua hilo. [3]

Endelea. Anza kumsifu Bwana” unaona, kwa sababu liko katika akili zao mpaka lije katika nafsi zao. [4]

Sasa usifikirie hili ni geni kwa habari hii, kwa maana Paulo aliweka kielelezo chini ya mkono wa Mungu. Paulo peke yake ndiye aliyekuwa na ufunuo mkamilifu kwa siku yake kama inavyo dhihirishwa na vile alivyokabiliana na mitume wengine ambao walikiri kwamba Paulo alikuwa Nabii – Mjumbe kwa watu wa mataifa wa siku ile. Na pia uone ule utambulisho unao elelezwa katika neno, kwamba Paulo alipotoka kwenda Asia Mungu alimkataza, kwa maana kondoo (watoto wake) walikuwa makedonia na wale (Wamakedonia) wangesikia kile ambacho Roho angesema kupitia Paulo, wakati watu waliokuwepo Asia wasingesikiliza (Matendo 16:6-12).

Katika kila wakati tunacho kielelezo hicho hicho. Hiyo ndiyo sababu Nuru inakuja kupitia Mjumbe – aliyechaguliwa na Mungu kutoka mahali fulani, na sasa kupitia mjumbe huyo ndipo Nuru inaenea kuingia kwenye huduma za wengine ambao wamefundishwa kwa uaminifu.

Lakini ni kweli kwamba hawa wengine wanaoenda nje siyo siku zote wanajifunza ilivyo muhimu kusema Tu kile mjumbe alichosema (2Timo3:10-17, 1Kor.4:6-7). (kumbukeni, Paulo aliwaonya watu waseme tu kile alichokisema, 1Korintho 14:37, mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohani, na ayatambue hayo ninayo maandikia, ya kwamba ni MAAGIZO YA BWANA. Au Je! Neno la Mungu lilitoka kwenu? Au kuwafikia ninyi peke yenu?) wanaongeza hapa, au wanaondoa hapa, na baada ya muda mfupi ule ujumbe sio usiochanganywa tena, na uamsho unakufa. Inatupasa kuwa waangalifu kuisikia sauti ile moja, kwa maana Roho ina sauti moja ambayo ni sauti ya Mungu (Yohana 10:27-30). Paulo aliwaonya watu waseme tu kile alichokisema kadhalika hata Petro, Aliwaonya watu kwamba hata yeye (PAULO) asingeweza kubadilisha neno moja la yale aliyoyatoa kwa ufunuo (Wagalatia1:6-12). Oh Jinsi ilivyo muhimu kuisikia sauti ya Mungu kwa njia ya wajumbe, na kusema kile walichopewa na kuyaambia Makanisa. [5]

Sehemu kubwa ya Imani yetu ni Imani ya kiakili. Kwa kusikia neno linalotuleta sisi kwenye ufahamu wa kiakili wa kumtambua mungu. Lakini kama ile itokayo juu, Oh, ndugu kama itagusa hii Unaona pale ile ya kimungu Imani ya kiroho. Sasa imani hii inafanya nini? Imani hiyo inatambua tu Neno. Haijalishi kitu kingine kinasema nini, inatambua tu Neno, kwa sababu “Hapo mwanzo kulikuweco neno, naye neno alikuwako kwa Mungu. Naye neno alikuwa Mungu. (Naye neno bado ni Mungu). Naye neno akafanyika mwili akakaa kwetu” (Yohana 1:1-3,14) na Neno lenyewe linajimwaga katika Imani yetu, Imani yetu ya kiakili na kuwa ufunuo wa kiroho. Na juu ya mwamba huu. Sio katika akili za kuwazia kujiunga na Kanisa, akili za kuwaza kitu kama hicho, lakini juu ya ufunuo. Wakati hiyo mito ya Neema imemwagikia katika imani ya kiakili ambayo unayo, sasa juu ya hilo, ufunuo wa kiroho, nitalijenga Kanisa langu na wala milango ya kuzimu haitalishinda” Unaona? Hiyo inaonyesha itakuwa kinyume nalo lakini haitaweza kulishinda. Oh, ni kitu cha utukufu sana. [6]

Na pia inasema kwamba wala hawezi mtu kusema, Yesu ni Kristo isipokuwa ni kwa ufunuo tu wa Roho Mtakatifu ambao umefunuliwa kwake (1kor. 12:3). Unaona? Natunasimama hapo, hakika tunarudi nyuma kwenye jambo lile tena, tunaangukia tena katika ufunuo. Ni lazima liwe limefunuliwa.

Wakati Yesu alipoulizwa hapa katika Matayo 16:17 na 18.. hatuna muda wa kusoma, lakini kama unataka kuliandika chini. Alisema watu wanasema mimi mwana wa Adamu kuwa ni nani? Mmoja wao alisema, “wewe ni Musa, Eliya, au mmoja wa manabii”.

Akasema, lakini nanyi mwaninena kuwa ni nani?

Akasema, “wewe ndiwe Kristo, mwana wa mungu aliye hai”

Akasema, “Umebarikiwa wewe, Simoni, mwana wa Yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili. Bali baba yangu aliye mbinguni ndiye aliyekufunulia hili na juu ya mwamba huu...” Ufunuo wa Kiroho wa Mungu ni nani, Yesu ni nani, Naye ni ufunuo wa Mungu, Mungu akiwa amefanyika mwili. Naye akafunuliwa kwa ulimwengu. Alikuwa ulimwenguni, Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake (2Kor. 5:18-19), alifunua vile Mungu alivyo katika mwili wa nyama. “Wewe ni Kristo, mpakwa mafuta, mwana wa Mungu.” Alisema, mwili na damu kamwe havikukufunulia hili, bali baba yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili juu ya mwamba huu, nitalijenga Kanisa langu Ufunuo wa neno kwa majira yake).

Kitabu cha ufunuo ni kitabu cha mwisho cha Biblia. Kimefungwa kwa wasioamini. Pale Biblia inasema ufunuo sura ya 22 “mtu yeyote akiondoa neno moja kutoka humo au akiongeza neno moja katika (maneno ya unabii wa kitabu hiki) Mungu atamwondolea sehemu yake katika kitabu cha uzima” tunafahamu sasa kwa jumla kilitolewa kwa ajili ya waaminio. Na inafungua kitabu cha ufunuo na kumfunua yule mwenye kitabu hicho chote ni (ataonekana kama Alpha na Omega, kutoka mwanzo hadi ufunuo, Yesu Kristo yule yule hasa sehemu zote), na hufunua siri yake yote na mpango wake kwa nyakati zote za Kanisa zijazo na zilifungwa pale na mihuri saba.

Sasa, kitabu kiliandikwa, lakini kumbuka, kilikuwa kimefungwa na mihuri saba. Na mihuri hiyo saba ilikuwa isifunguliwe, ufunuo 10, mpaka wakati wa baragumu ikipigwa ya Malaika wa mwisho wa dunia Ufunuo 10:7 Unaona? Na katika siku za sauti ya ujumbe wa mwisho wa Malaika wa saba, Siri ya Mungu itakuwa imekwisha katika wakati huo. Na huo ndio wakati ambao tunaishi ndani yake.

Wote tunajua kuwa tunaishi wakati wa Loadikia (Ufunuo 3:14-21). Hakutakuwa na wakati mwingine. Kwahiyo tunaishi katika wakati wa Loadikia, na hii mihuri saba ambayo imeshikilia hiki kitabu ni siri kwa watu, nacho kitafunguliwa katika siku ile. Hivyo ndivyo alivyo ahidi sasa haiwezi kuwa kitu chochote nje ya Neno, kwa sababu huwezi kuongeza katika Neno au kupungua kutoka katika Neno. Inabidi ibakie siku zote ni Neno. Lakini ule ufunuo utafunua ule ukweli, ni kitu gani, kuifanya

ikubaliane na maandiko mengineyo. Na hapo Mungu atathibitisha kwamba hiyo ni kweli.

Unaona, Mungu hahitaji mtafsiri. Yeye ni mtafsiri wake mwenyewe. Anafanya tafsiri yake mwenyewe, kwa kuvifanya vitokee vile ambavyo amesema vitatokea. Kama vile mwanzo alisema, “Na iwepo nuru”, na nuru ikawepo (Mwanzo 1:3-5). Hiyo haitaji mtafsiri yeyote. Ilihithibitishwa. [7]

Kumbuka, Yesu alizungumza na watu waliokuwa waaminifu, waabudu wa siku zake, na Alisema, “Mnaniabudu bure” (Marko 7:1-9). Ni kweli, Ibada halisi kutoka kwenye mioyo yao, Mnaniabudu bure mimi, mkifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya watu,” au kanuni za madhehebu zao, kwa uaminifu, kwa heshima, wakiwa wakidini kama wawezavyo kuwa, na hiyo haikuwa mpya kwamba ni mafarisayo tu. Kaini na Habili, waabuduo wa kwanza ambao walizaliwa kinamna ya asili hapa duniani kwa hakika kabisa walikuja na mtazamo huo huo.

Kaini alikuwa wakidini kama habili alivyokuwa. Wote walijenga madhabahu. Wote walimpenda Mungu. Wote walitoa sadaka, wote waliabudu, wote walitoa fungu la kumi. Wote walifanya kila kitu sawasawa. Lakini Habili kwa Imani, ambayo ni ufunuo Neno la Mungu lililofunuliwa, likawekwa wazi, likaonekana na kuthibitishwa.....Utukufu! Kaini alitengeneza matoleo, lakini Mungu hakuyathibitisha, Mungu alitaka kuabudiwa na Kaini akatoa dhabihu, lakini Mungu hakuithibitisha hiyo. Lakini kwa njia ya kweli....

Unasema, “Vema, Kanisa langu ni, jamani.....”

Subiri kwa dakika. Mungu hutafsiri neno lake kwa namna ile lilivyonenwa. Unaona? Kaini alisema, “Mimi ni wakidini. Mimi ninampenda Muumba wangu. Nakutolea ee Mungu madhabahu hii yakupendeza nakutolea wewe sadaka hii. Nimejenga vitu hivi vyote Bwana, kwa sababu ninakupenda wewe” Habili alisema mambo hayo hayo. Sasa ni ile inayothibitishwa, ile inayokubaliwa. Na Mungu alishuka chini na akaipokea sadaka ya Habili, kwa sababu ya ufunuo aliifikia njia ya kweli ya Mungu inayokubalika.

Sasa, uangalie ile roho ya Kaini inayoshuka hapa chini kupitia maandiko, inavyoendelea hata siku hizi za mwisho, namna ya kiasili? Kiasili tu kama ile nyingine ilivyokuwa.

Mwangalie yule nabii Balaam na nabii Musa, wote wawili wakiwa na madhabahu saba (hesabu 23:27-30), madhabahu za Yehova, damu ilikuwepo katika kila moja na siyo hivyo tu, lakini Kondoo mume katika kila moja kwa namba, namba iliyo sahihi, saba kamilifu, kondoo dume saba, ilikuwa sawa kabisa katika madhabahu zote mbili. Kwa msingi ule ule mmoja alivyofanya, ndivyo na mwingine alivyokuwa pia. Lakini ni yupi Mungu alimthibitisha? Yule mmoja aliyekuwa katika Neno lake. Ile ya kimsingi haimanishi sana ni ule ufunuo wa Mungu. [8]

Kaini aliwaza Mungu anakaa katika uzuri wa dunia. Alifanya hivyo Mbinguni. Dhambi haikuanza bustani ya Edeni, ilianza Mbinguni wakati lusiferi mwana wa asubuhi alijiinua mwenyewe katika uzuri na akitaka ufalme ulio mzuri zaidi ya ule wa Mikaeli na alifikiri kwamba Mungu alikaa katika uzuri (Ezekieli 28:11-17)

Na tumwangelie Kaini. Hakutaka sadaka ya damu. Alikuwa pale na kutoa matunda ya Shambani yakupendeza katika madhabahu yake. Wa kidini sana, alifanya kila kitu hasa kama Habili alivyofanya. Alitoa sadaka, alianguka chini mbele za Mungu akiabudu, mtiifu katika kila njia, lakini hakuwa na ufunuo wa lile Neno. Na neno lilikuwepo tangu mwanzo, mpango wa Mungu. Lakini Mungu alifunua kwa ufunuo jambo lile hasa yeye alilolithibitisha na kulikubali kwamba ni sahihi. Siyo dini, siyo madhehebu, siyo kuwa mwanachama wa kanisa, siyo kutoa sadaka, siyo kuwa mwaminifu, lakini ni kwa ufunuo wa Neno la Mungu, Mungu akimfunulia yeye kwamba mama yake hakula tunda alilopewa na nyoka, lakini alitenda zinaa na utu wa nyoka katika umbile la mnyama, wala siyo aina ya mnyama anayetambaa lakini ni mjanja sana, mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu, yuko katika sura ya mtu, na ni wa pekee ambaye mbegu zingeweza kuchanganyika. Sasa, sayansi inajaribu kumpata yeye na bado hawataweza kumpata, kwa sababu kila mfupa katika mwili wake ulibadilishwa. Lakini Biblia inadai kuwa ndiye (mwanzo 3:1-7).

Unaona roho hizo mbili zinazopingana zikiwa kazini katika kizazi hiki kiovu? Unaweza kuona hilo? Kila moja ikiwa ni ya kidini sana Kaini na Habili, zile roho zikiwa zimekomaa kufikia vichwa vyao, bado ziko vilevile kama zilivyoanza. Mmoja akiabudu kwa uzuri na kwa maarifa na kwa elimu na kwa sayansi na kwa elimu za maadili na ile nyingine, kwa Imani ya ufunuo wa Neno la Mungu.

Lakini Bibi Arusi ni sehemu ya Bwana arusi, mkweli kwake katika kila jambo akisubiri siku ya kufungiwa ndoa, wakiungana, siyo kwenye baraza la Makanisa, lakini kule mawinguni, kwenye karamu ya arusi (1Thess 4:15-17). Yeye amepewa na imefunuliwa kwake ile siri ya mihuri saba ya Biblia. Anaona ujinga wake mdanganyaji, akiwa karibu sana na ukweli kiasi cha kumdanganya aliye mteule kama ingewezekana (Matayo 24:24) naye analiona hilo. [9]

Lakini kwa Kanisa, Bibi arusi unyakuo ni ufunuo wake. Imefunuliwa kwake, kwamba ufunuo, Bibi arusi wa kweli atakuwa akingojea huo ufunuo wa unyakuo.

Sasa, ni ufunuo, kwa maana ufunuo ni Imani. Huwezi, ukawa na ufunuo bila ya huo kuwa ni Imani. Imani ni ufunuo kwa sababu ni kitu fulani kinachofunuliwa kwako. Imani ni ufunuo. Imani ni kitu fulani ambacho kimefunuliwa kwako kama ilivyokuwa kwa Ibrahimu, ambacho kingeita kitu chochote kilicho kinyume na kile kilicho funuliwa kwake kwamba hakipo/hakikuwa hivyo (Rumi4:16-22). Sasa Imani ndivyo imani ilivyo ni ufunuo wa Mungu. Kanisa linajengwa juu ya ufunuo, mwili wote mzima. [10]

Sasa kuna vitu vitatu ambavyo watu wanaishi kwa hivyo moja ni ile ya kibinadamu. Pili ni ufunuo wa kiungu. Na tatu ni maono.

Sasa, hii kama kwenye maombi unapomuomba mtu yeyote kwa jinsi ya kibinadamu, tunasema, “Vema, natumaini utapata kupona. Unaona, ninatumainia. Ninaamini pamoja na wewe, kujaribu kutumia imani yote niwezayo” Hiyo ni ya kibinadamu.

Pili ni ufunuo wa kiungu, jambo fulani linapofunuliwa kwako unajua hivyo moyoni mwako kwamba hilo litatokea, na bado hakuna chochote ila ufunuo. Tatu ni maono. Kwa sababu hayo ni HII ASEMA BWANA. Hiyo ni kamilifu na ya hakika. [11]

Unaona: Hapa ipo siri, Siri ni maandiko ni ukweli uliofichika kwanza, na sasa unafunuliwa kiungu, lakini bado inabakia kitu cha kimiujiza ndani yake, pamoja na kufunuliwa. [12]

Siri yake inafunuliwa tu kwa Bibi arusi wake mpenzi, Huyu tu ndiye pekee awezaye kuiona hiyo. [13]

Naamini ni Yesu alisema kwa Pilato, jambo fulani nilikuwa nikilifikiri na Alisema pale muda mfupi uliopita, “Nani alikuambia hilo?” Au “limefunuliwa kwako? Ulijuaje mambo haya?” Kwa maneno mengine sikumbuki hasa lile neno ni neno gani sasa, ni muda mrefu tangu niliposoma hilo, lakini “umelitambua hilo..... kwa namna gani.... Nani amefunua hili kwako?” Ni juu ya yeye kuwa ni mwana wa Mungu. “Na amekufunulia wewe hili? Je ni mtu fulani amekuambia hilo? Au kama Yesu alivyosema, je ni Baba yangu aliye Mbinguni amekufunulia wewe? Umelisoma wapi? umeambiwa na mtu au ni ufunuo mkamilifu kutoka kwa Mungu? (Yohana 18:28-40)

Huu Ushirika ni kitu nimekiamkia/nimekifanya, kama agizo na kusema “Vema wengineo wote wanashiriki hiki, nami nitashiriki pia?”

Ni ufunuo kwamba mimi ni sehemu yake na ni sehemu yako, nami ninakupenda wewe na ninampenda yeye, na tunashiriki huu pamoja kama ishara ya upendo wetu kwa Mungu, na upendo wetu na ushirika wetu mmoja kwa mwingine. [14]

Hakuna mtu ajuaye mambo ya Mungu ila Roho wa Mungu na yoyote ambaye Roho wa Mungu apenda kuwafunulia wao. Tunahitaji tumuomba Mungu kwa ajili ya ufunuo zaidi kuliko kitu kingine chochote duniani. Tumeikubali Biblia, tumekubali kweli zake zilizokuu, lakini bado siyo halisi sana kwa wata wengi kwa sababu ufunuo wa Roho haupo pale. Lile neno halijahuishwa. [15]

Hatupaswi kugeuza watu wawe wakristo kwa kutumia serikali, lakini kwa ufunuo wa Kristo ndani yako, kama Mungu alivyokuwa ndani ya kristo, kristo ndani yako (Wakolosai 1:26-29). Kile Mungu alichokifanya ndani ya Kristo, Kristo anakifanya ndani yako. Ishara Mungu alizozifanya ndani ya Kristo, Kristo anazifanya ndani yako. Oh, si linapendeza hilo? Yesu alisema siku ile (Yohana 14:19-20) – hiyo

ilikuwa leo – katika siku ile wakati ufunuo huu utakapofahamika, mtajua kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani yangu, na mimi ndani yenu nanyi ndani yangu, wakati ufunuo utakapohitaji kudhihirishwa katika siku hiyo, utajua ya kuwa mimi na Baba tu mmoja. Niko ndani ya Baba na Baba yuko ndani yangu. Sasa wakati ufunuo unapoendelea kuja itakuwa sasa ni mimi ndani yenu na ninyi ndani yangu. [16]

Nukuu za Kiingereza

- [1] Nimesikia bali sasa ninaona (kitabu cha 7na 3), aya 55-57
- [2] Yehova-Yire sehemu ya 1 aya 38
- [3] Matendo ni Imani iliyodhihirishwa Aya 105-107, 126, 128, 115-118, 186,327.
- [4] Sura za Yesu (59-0525), Aya 14
- [5] Wakati wa Kanisa la simirnaa kitabu cha nyakati saba uk. 156.
- [6] Majina ya makufuru uk. 19+22.
- [7] Unyakuo Aya 69-77
- [8] Mahali Bwana alipopachagua pa kuabudia (kitabu cha 7 na 4) Aya 81-86.
- [9] Mungu wa kizazi hiki kiovu Aya 80-81, 164.
- [10] Unyakuo Aya 65
- [11] Safina (kitabu cha 26 na 18) Aya 6-9
- [12] Je huu ni wakati wa mwisho Bwana? Uk. 30-31
- [13] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa uk. 71.
- [14] Ushirika kitabu cha 18 na 4 Aya 63
- [15] Ufunuo wa Yesu Kristo kitabu cha nyakati saba za Kanisa uk 31.
- [16] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa uk. 65

Jiwe la kiroho la kujengea na. 150 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia. (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

*Charles E. Y. Kanju,
Box 553 Korogwe - Tanga
E-mail: Chaelika@live1.com
Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*